## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Matokeo ya mtihani wa Kiswahili yamekuwa yakiyumba mwaka baada ya mwingine tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya.Watahini wamekuwa wakishuhudia kushuka kwa viwango vya majibu yanayotolewa na watahiniwa .Kadhalika, kumekuwa na kushuka na kupanda kwa asilimia ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka minne (2011 hadi 2014 )

**Jedwali 10: Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (2011 – 2014)**

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 1 | 410,807 | 40 | 16.43 | 5.61 |
| | 2 | | 80 | 43.45 | 13.18 |
| | 3 | | 80 | 37.76 | 14.96 |
| | Jumla | | 200 | 97.63 | 29.81 |
| 2012 | 1 | 433,886 | 40 | 10.43 | 3.63 |
| | 2 | | 80 | 29.06 | 10.77 |
| | 3 | | 80 | 32.14 | 15.15 |
| | Jumla | | 200 | 71.62 | 25.71 |
| 2013 | 1 | 445555 | 40 | 18.46 | 5.44 |
| | 2 | | 80 | 29.92 | 12.68 |
| | 3 | | 80 | 34.82 | 14.92 |
| | Jumla | | 200 | 83.19 | 29.77 |
| 2014 | 1 | 482122 | 40 | 20.17 | 5.26 |
| | 2 | | 80 | 32.27 | 12.60 |
| | 3 | | 80 | 42.93 | 15.81 |
| | Jumla | | 200 | 95.36 | 29.88 |

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

(i) Alama ya wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) ya mwaka wa 2014 imepanda kutoka **18.46** mwaka 2013 hadi **20.17** mwaka huu.

(ii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **37** sawa na na **37** mwaka 2013. Ni mtahiniwa **mmoja** tu aliyepata alama hii.

(iii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi katika karatasi hii ni **20** ikilinganishwa na **17** ya mwaka 2013. Watahiniwa **35,106**, ndio waliotuzwa alama **20.**

(iv) Karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Hili linadhihirishwa na alama tenganisho **(5.26)** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na

alama ya tenganisho ya kikaida **(15.00)**. Hali hii inaweza kusababishwa na watahini kuongozwa na kutawaliwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa, na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

(v) Alama ya wastani ya karatasi ya pili imepanda kutoka **29.92** ya mwaka 2013 hadi **32.27** mwaka 2014.

(vi) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **75** ikilinganishwa na **74** ya mwaka 2013. Ni mwanafunzi **mmoja** tu aliyetuzwa alama hii.

(vii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi katika karatasi hii ni **30** ikilinganishwa na **25** ya 2013. Watahiniwa **14,052** ndio waliotuzwa alama hii.

(viii) Karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ni **12.60.**

(ix) Utendaji wa watahiniwa katika karatasi ya pili (102/2) umeimarika kiasi.Hata hivyo, matokeo haya bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha. Matokeo ya karatasi hii yamezidi kuyumba tangu mwaka wa 2009. Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi (10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta thelathini (14.30)** mwaka 2012. Mwaka 2013 ilipanda kwa kiasi kidogo mno, na mwaka huu ikapanda kwa alama 2.35.

(x) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2014 yamepanda sana; kutoka **34.82** mwaka 2013 hadi **42.93** mwaka huu .

(xi) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **79** sawa na **79** ya mwaka 2013. Ni watahiniwa **wanane** tu waliotuzwa alama hii.

(xii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi ni **50** ikilinganishwa na **36** ya mwaka 2013 . Watahiniwa **12,179** ndio waliotuzwa alama hii.

(xiii) Alama wastani ya somo la Kiswahili kwa jumla imeimarika kutoka **83.19** mwaka 2013 hadi **95.36** mwaka 2014.

(xiv) Asilimia ya watahiniwa wanaopata gredi A na A- ni ndogo mno.

(xv) Alama wastani ya somo hili bado haijafikia kiwango cha kuiridhisha.

## 3.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

### 3.2.1 Kiswahili Insha (102/1)

**Jedwali 5: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2011 – 2014**

| Mwaka | **2011** | **2012** | **2013** | **2014** |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 16.43 | 10.43 | 18.46 | 20.17 |
| Alama ya Tenganisho | 5.61 | 3.63 | 5.44 | 5.26 |

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa kipindi cha miaka miwili (2013-2014), utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umekuwa ukiimarika.Tathmini ya kazi halisi za watahiniwa imebainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa sasa inamudu kujieleza kwa lugha iliyokomaa zaidi ikilinganishwa na miaka ya awali. Kadhalika idadi ya watahiniwa wanaopata alama za chini zaidi imepungua.Hata hivyo, bado kuna asilimia kubwa ya wanafunzi wanaopata chini ya nusu ya alama zilizotengewa karatasi hii. Imebainika pia kwamba idadi ya watahiniwa waoteua swali linalohusianana methali imeongezeka.Hili linadokeza kwamba ule mtazamo wa kijadi kuwa insha zinazohusiana na methali huwa ngumu umeanza kubadilika.

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.

**1 Lazima**

Andika hotuba utakayowatolea wazazi, walimu na wanafunzi kuhusu umuhimu wa ushauri-nasaha katika shule za sekondari.

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika hotuba kuhusu umuhimu wa ushauri nasaha katika shule za upili..Watahiniwa wengi walimudu kuzingatia muundo wa nje wa utungo wa aina hii.

Hata hivyo,tungo za watahiniwa zilidhihirisha kwamba wengi wamekosa ubunifu.Wengi hawakuelewa maana ya ushauri nasaha, hivyo hawakuweza kujadili hoja zilizotarajiwa; wakashindwa kukuza mada kikamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawasomi kwa mapana , hivyo hawadiriki kushughulikia masuala ibuka ipasavyo katika tungo zao.

#### 3.2.1.1 Ushauri kwa walimu

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Elimu.

#### 3.2.1.2 Mapendekezo

(i) Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.

(ii) Walimu watumie silabasi ya KICD ili kuelekeza ufundishaji wao. Mwongozo unaotolewa na KNEC kuhusu mada na stadi zinazotahiniwa, pamoja na vitabu vya fasihi vinavyotahiniowa, utumiwe kujalizana na silabasi ya KICD.

(iii) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana, na kwa kina (magazeti, majarida, kazi za kifasihi, na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa. Hili litapalilia ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala nyeti/masuala ibuka iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.

(iv) Wanafunzi wahamasishwe kufasiri maswali kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

### 3.2.2 Kiswahili Lugha (102/2)

**Jedwali 6: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2011 hadi 2014**

| **Mwaka** | **2011** | **2012** | **2013** | **2014** |
|---|---|---|---|---|
| **Alama ya Wastani** | 43.45 | 29.06 | 29.92 | 32.27 |
| **Alama ya Tenganisho** | 13.18 | 10.77 | 12.68 | 12.60 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yamepanda mwaka wa 2014 kwa alama 2.35.
Swali la kwanza na la pili ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa zaidi, ingawa wengi pia walipoteza alama katika swali la tatu na la nne.Tutachanganua swali la tatu.

**Swali la 3 : MATUMIZI YA LUGHA**

**MATUMIZI YA LUGHA:** (Alama 40)

(a) (i) Eleza maana ya silabi. (alama 2)

(ii) Andika neno lenye muundo ufuatao: (alama 1)

irabu + konsonanti + konsonanti + irabu

(b) Ainisha vitenzi katika sentensi: (alama 3)

Ndege <u>yu</u> taabani, hata hivyo <u>anajaribu</u> <u>kujinasua</u>.

(c) Geuza sentensi ifuatayo kwa kufuata maagizo. (alama 2)

Wachezaji hawakucheza mpira kwa sababu ya mvua.
Anza kwa: Mpira

(d) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu.

Dobi huwapigia watu nguo pasi. (alama 2)

(e) Andika sentensi ifuatayo upya ukizingatia kinyume cha maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

<u>Ubora</u> wa kazi zao <u>ulifichika</u> <u>baada ya</u> <u>kuanzishwa</u> kwa mradi ule.

(f) (i) Eleza maana ya kirai. (alama 2)

(ii) Ainisha virai vilivyopigiwa mstari. (alama 1)

Zana hizi zimeundwa na mafundi wenye ustadi mkubwa.

(g) Kinga ni hali ya kuzuia madhara fulani. Andika maana nyingine **mbili** za 'kinga'. (alama 2)

(h) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha matawi. (alama 2)

Lililimwa vizuri sana.

(i) Bainisha maana **mbili** zinazojitokeza katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wakimbizi walisema kuwa walitamani kurudi kwao mwaka huo.

(j) Eleza sifa **mbili** za sauti ifuatayo: **dh**. (alama 2)

(k) Andika sentensi ifuatayo katika umoja. (alama 2)

Hao wenyewe hawakuzingatia mafunzo ya lishe bora.

(l) Tunga sentensi **moja** kubainisha tofauti ya kimaana kati ya **gharama** na **karama**. (alama 2)

(m) Kanusha sentensi ifuatayo: (alama 2)

Wanafunzi waliingia darasani, wakatoa vitabu wakaanza kusoma.

(n) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** tofauti ya nukta pacha. (alama 2)

(o) Tumia nomino ya jamii kuwakilisha maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 1)

Nzige wengi sana walivamia na kuharibu mimea.

(p) Onyesha visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari. (alama 2)

Washiriki wote walituzwa medali baada ya mchuano huo.

(q) Nomino zifuatazo zimo katika ngeli gani?

(i) Furaha (alama 1)

(ii) Nyasi (alama 1)

(r) Unganisha sentensi hizi ukitumia kiunganishi cha kinyume. (alama 2)

Wananchi walikabiliwa na hatari.
Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

(s) Andika upya sentensi ifuatayo ukianzia kwa yambwa tendwa. (alama 2)

Wafugaji waliwakatia ng'ombe wote majani ya mti huo.

Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi. Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi kujibu maswali aliyopewa. Watahiniwa wengi sana walishindwa kumudu dhana za kimsingi za kisarufi kama vile kuandika katika umoja, aina za viarai, na uchanganuzi wa sentensi ya kimsingi.. Wengine walishindwa kujibu maswali ya kimsingi ya mtamshi bora.Kadhalika ,watahiniwa wengi mno walipoteza alama katika maswali yote, hata ya ufahamu na ufupisho kutokana na makosa ya sarufi na hijai. Wengine hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo.

3. (a)

(i) Silabi ni kipashio cha utamkaji ambacho hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti. **mf nda - ma** ; katika : ndama (alama 2)

**Au**

Ni sauti moja au zaidi zinazotamkwa kama fungu moja la sauti / kama sauti moja.
Mf. o - a katika oa

2/0 - (alama 2)

(ii)

| | | |
|---|---|---|
| afya | enda | upwa |
| anza | anga | igwa |
| ibra | uzwa | |

1 x 1 = (alama 1)

(b) yu - kitenzi kishirikishi / kishirikishi kipungufu
anajaribu - kitenzi kisaidizi
kujinasua - kitenzi kikuu

3 x 1 = (alama 3)

(c) Mpira haukuchezeka kwa sababu ya mvua nyingi.

au

Mpira haukuchezwa na wachezaji kwa sababu ya mvua nyingi. 2/0 - (alama 2)

(d) Dobi atakuwa amewapigia watu nguo pasi. 2/0 - (alama 2)

(e) **Udhaifu** wa kazi zao **ulifichuka** **kabla ya** **kusitishwa** kwa mradi ule.

(Kumalizwa)
(Kukamilishwa)
(Kuhitimishwa)
(Kukomeshwa)

($\frac{1}{2}$ x 4 = alama 2)

(f) (i) Kirai ni fungu la maneno ambalo hudokeza maana lakini maana hiyo si kamili.

**au**

Kirai ni fungu la maneno ambalo huainishwa kwa kuzingatia neno lake kuu. Kwa mfano, nomino ndilo neno kuu la kirai nomino.

(ii) (a) na mafundi - kirai husishi/kirai kihusishi.

(alama 2)


(b) wenye ustadi mkubwa - kirai kivumishi / kirai vumishi

(alama 1)
$2x\frac{1}{2} = 1$

(g) Kinga ni jambo au dawa ya kujiepusha na madhara.
Kinga ni kipande cha ukuni chenye moto.
Kukinga ni kutayarisha bindo, mkono au chombo ili kupokea kitu.

(1 x 2 = alama 2)

(h)




$(8 \times \frac{1}{4}$ = alama 2)

(i) (i) Wakimbizi ndio wanatamani.
(ii) Watu wengine wanatamani.
(iii) Wakimbizi watarudi nyumbani kwa wakimbizi.
(iv) Watu wengine watarudi kwao (hao wengine).
(v) Watu wengine watarudi kwa wakimbizi.

(2 x 1 = alama 2)

(j) dh + kikwamizwa / kikwaruzo
+ ghuna
+ menoni

(2 x 1 = alama 2)

(k) Huyo mwenyewe hakuzingatia funzo la lishe bora.

$4 \times \frac{1}{2}$ =(alama 2)

(l) Maana zifuatazo zijitokeze:
Gharama (i) jumla ya bei ya kufanyia jambo/pesa zinazohitajika kufanya jambo.
(ii) unalopoteza kwa kutozingatia maagizo.

Karama - kipawa kutoka kwa Mungu.

2 x 1 (alama 2)

(m) (i) Wanafunzi hawakuingia darasani wala hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.
(ii) Wanafunzi hawakuingia darasani, wakatoa vitabu na kuanza kusoma.
(iii) Wanafunzi hawakuingia darasani na hawakutoa vitabu wakaanza kusoma.

2/0 - (alama 2)

(n) Nukta pacha

(i) Hutumiwa kutanguliza maneno halisi ya msemaji.
Mwalimu: Nawashauri msome kwa bidii.
Wanafunzi: Tunashukuru.

(ii) Hutumiwa kutanguliza maneno yaliyo kwenye orodha.
Alienda sokoni kununua: mapera, machungwa na papai.

(iii) Kutenga saa na dakika - saa 8 : 30

(iv) Kutenga shilingi na senti: Shilingi 10:50

(v) Kutenga sura na mstari, Yohana 8:30

2x1

(o) **<u>Wingu</u>** la nzige

(p) Medali - nishani
Mchuano - Kinyang'anyiro, mchezo, mashindano, shindano, pigano.
(2 x 1 = alama 2)

(q) (i) Furaha - 1 - 1 (alama 1)
(ii) Nyasi - U - Z1/ Z1 (alama 1)

**Tanbihi**

Kuna baadhi ya watahiniwa ambao huenda wakatumia uainishaji wa ngeli unaozingatia viambishi awali vya nomino. Hawa pia watuzwe ipasavyo. Kwa mfano:

(i) Furaha - N - N
(ii) Nyasi - U - N / U - NY / N

(r) Mf

(i) Wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi **licha ya** kukabiliwa na hatari.
(ii) **Pamoja na** hatari iliyowakabili, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.
(iii) **Minghairi ya** kukabiliwa na hatari, wananchi waliendelea kuwaokoa majeruhi.

Mifano mingine: hata baada ya, ilhali, lakini, bali, bighari ya, ila

(s) **Majani ya mti huo** yalikatiwa ng'ombe wote na wafugaji.
Yambwa (tendwa) (alama 2)

**MAPENDEKEZO**

(i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi.

(ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi/ utekelezaji na usanisi .Wasitarajie kila mara kupata maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye vifungu au kukariri kutoka kumbukumbu zao.

(iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku mtiririko ufaao ukisisitizwa ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

(iv) Walimu wasisitize vipengele vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.

(v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe zaidi. Mathalan mwalimu anaweza kutumia fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.

(vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.

(vii) Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

### 3.2.3 Kiswahili Fasihi (102/3)

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2011 hadi 2014.

| Mwaka | 2011 | 2012 | 2013 | 2014 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 37.76 | 32.14 | 34.82 | 42.93 |
| Alama ya Tenganisho | 14.96 | 15.15 | 14.92 | 15.81 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii umeimarika zaidi mwka huu. Hata hivyo tathmini ya karatasi halisi za watahiniwa ilibainisha kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa, hata wale wanaopata alama za juu zaidi katika karatasi hii, haimudu kuwasilisha hoja kwa lugha sahihi na komavu. Kazi za watahiniwa zimepwezwa na makosa mengi ya kisarufi, kimuundo na hijai.Kadhalika, pameibuka mtindo wa kuwasilisha hoja kwa ufupi mno, kiasi cha kuwawafanya baadhi ya watahiniwa kupoteza alama.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.

**K. Walibora:** *Kidagaa Kimemwozea*

"Labda ni suala la mzigo wa mwenzio kanda la usufi."
"....Sijui 'mwenyewe' aliyetajwa ... ni nani. Lakini sharti awe mtu ambaye kwake msiba kwa wengine kwake arusi."

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Bainisha tamathali **mbili** za usemi zinazojitokeza katika dondoo hili. (alama 2)

(c) Jadili jinsi ambavyo hali ya, 'msiba kwa wengine kwake arusi', inavyojitokeza katika *Kidagaa Kimemwozea.* (alama 14)

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa:

a) kutumia uelewa wake wa ploti kujibia swali
b) kutumia ujuzi wake wa vipengele vya kimtindo kubainisha tamathali za usemi zilizotumiwa katika dondoo alilopewa
c) kuoanisha yaliyomo katika dondoo na masuala mengine yanayohusiana na wahusika wengine katika riwaya.

Hata hivyo, ilidhihirika kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haifahamu dhana ya tamathali za usemi Kadhalika, watahiniwa wengine walijadili mbinu za utawala badala ya mbinu za kimtindo
Pia ilibainika kwamba watahiniwa wengi bado wana mtazamo hasi kuhusu ushairi. Ni watahiniwa wachache tu waliofanya maswali ya ushairi.Watahiniwa hawa hawakupata alama za juu.

1. (a) (i) Kauli ya kwanza ni ya Amani kwa Imani.
(ii) Kauli ya pili ni ya Imani.
(iii) Anamwambia Amani.
(iv) Anamhadithia Amani kuhusu kadhia iliyompata; kupigwa kwa mama yake, kufa kwa mama yake, na kuchomewa nyumba, kisha kukashifu hali ya wanakijiji cha Baraka kutotenda lolote kumtetea.
(v) Wamo kibandani mwa Amani.
(vi) Imani anashangaa ni nani aliyewatuma askari kutekeleza matendo haya ya kinyama.

4 x 1 = 4

**Tanbihi**
Dondoo limetolewa uk. 58.

(b) (i) **Kinaya** - mtu kufurahia msiba wa wengine.
(ii) **Tanakuzi** - msiba na arusi ni vinyume - kuonyesha uovu/ugumu wa moyo.
(iii) **Sitiari** - msiba - matatizo
- arusi - furaha
- mzigo wa mwenzio kanda la usufi - kudunisha matatizo ya wengine.
- msiba kwa wengine kwake harusi - kufurahia matatizo ya wengine.
(iv) **Methali**, "Mzigo wa mwenzio ni kanda la usufi", imedokezwa na kauli, 'Mzigo wa mwenzio kanda la usufi.'

2 x 1 = 2

(c) (i) Raia wa Baraka, badala ya kumpoza Imani kwa kuchomewa nyumba, wanaogopa hata kuonekana wakizungumza naye, wanaaendelea tu na shughuli zao.
(ii) Viongozi wanawadhulumu hata wasio na chochote. Nasaba Bora anawadhulumu akina Imani shamba lao na kujifaidi kwalo.
(iii) Nasaba Bora anamuua Chichiri Hamadi ili kunyakua mali yake.
(vi) Baadaye Yusufu anasingiziwa mauaji haya na anafungwa.
(v) Nasaba Bora anampagaza Amani malezi ya Uhuru huku akijua mtoto si wa Amani. Hata anamtarajia Amani kuendelea na kazi yake ya uchungaji pamoja na ulezi huu.
(vi) Nasaba Bora anashirikiana kimapenzi na msichana mchanga - Lowela - bila kujali mustakabali wake.
(vii) Nasaba Bora anakitupa kitoto chake mlangoni pa Amani ili kujitoa lawamani bila kuwazia afya yacho.
(viii) Nasaba Bora anamwachia mkewe upweke huku akitafuta raha kwa wasichana wadogo kama vile Lowela.
(ix) Nasaba Bora anampiga Amani kikatili kwa shutuma zisizo na ithibati na kumtupa; anachojali ni kulipiza kisasi tu.
(x) Fao anamwendea kinyume mwanafunzi wake kwa kuhusiana naye kimapenzi

bila kujali unyonge wake kama mwanafunzi. Anapomtunga mimba anaondoka bila kujali hali ya mtoto na mama yake.

(xi) Michelle anakataa posa ya Majununi hata baada ya Majununi kujikalifu kujenga jumba ili kutimiza masharti yake.

(xii) Majisifu anamwibia Amani mswada na kujifaidi kwao, hajali yatakayompata Amani.

(xiii) Majisifu, badala ya kuhudhuria madarasa, anaingilia ulevi bila kujali maendeleo ya wanafunzi wake.

(xiv) Wenzake Amani chuoni wanamsingizia uchochezi na kumfanya kufungwa na kukatiza masomo yake.

(xv) Nasaba Bora anawafungia Amani na Imani kwa madai kwamba wamekiua kitoto japo kimekufa kwa kichomi. Askari kuwabeza Amani na Imani.

(xvi) Wauguzi hospitali wanakosa kukitibu kitoto, wanasema ni sikukuu, hawafanyi kazi, na kusababisha kifo chacho, huku wakiendelea na shughuli zao.

(xvii) Serikali inawatelekeza wazalendo, kama vile Matuko Weye, hata anafungiwa anaposema ukweli kuwahusu viongozi.

(xviii) Nasaba Bora anamtaliki mkewe kwa shutuma ambazo hata hajathibitisha, licha ya kwamba mkewe amekuwa mwaminifu kwake. Yeye Nasaba Bora anaendelea na uhusiano wake na Lowela.

(xix) Serikali inawatelekeza wachezaji kama vile Makweche katika umaskini na ugonjwa hata baada ya kuiletea nchi sifa. Makweche anaishia kukatwa mguu.

(xx) Askari wanampiga mamake Imani machoni pake bila kujali dhiki ya kisaikolojia wanayomsababishia. Baadaye Mama Imani anakufa kwa maumivu haya.

(xxi) Oscar Kambona, baada ya kuuawa kwa mama yake, anaondoka bila kuaga, anamwachia Imani ukiwa.

(xxii) Wahudumu katika zahanati hawamshughulikii DJ. DJ analazimika kuondoka hospitali kutafuta matibabu kwingine.

(xxiii) Serikali, badala ya kufadhili elimu ya maskini, inatumia pesa hizi kudhamini elimu ya wanaojiweza kama vile Fao. Fao anapelekwa kusomea ng'ambo.

(xxiv) Nasaba Bora anawashurutisha raia kuchangia elimu ya mwanawe - Madhubuti, hajali hali yao duni kiuchumi. Madhubuti anakwenda kusomea Urusi.

(xxv) Majisifu anawadharau wanawe wenye mahitaji maalum. Anamwachia mkewe ulezi bila kujali dhiki anazomsababishia. Hawapeleki wanawe shuleni au kwa uangalizi maalum.

(xxvi) Nasaba Bora, badala ya kuwahudumia raia katika afisi za Wizara ya Ardhi anaficha faili na kuwalazimisha kutoa hongo ili kuhudumiwa.

(xxvii) Nasaba Bora hajali afya ya majibwa yake, hayachanji.

(xxviii) Nasaba Bora anawafuta wafanyakazi wake kiholela, hata kwa kunadhifisha maskani yake, hajali watapata wapi riziki.

(xxix) DJ kuumwa na jibwa na mtemi hajali.

(xxx) Mtemi kumpita mama anayejifungulia njiani huku mvua ikinyesha. Hajali kumsaidia hata anaponasihiwa na mkewe.

(xxxi) Wazungu kunyakua mashamba ya Waafrika.

(xxxii) Wazungu kuwakataza Waafrika kufuga na kupanda baadhi ya mimea.

(xxxiii) Mashaka kuwabeza watoto walemavu wa Majisifu.

(xxxiv) Majisifu anaposhindwa kutoa mhadhara wanafunzi wanamcheka /wanamkejeli.

**Tanbihi**

(i) Mtahiniwa anaweza kuonyesha:

Tendo la kikatili linaloelekezwa kwa mhusika au kundi fulani, kwa faida ya anayetenda tendo hilo,

**Au**

Aonyeshe hali ya mapuuza au dhuluma inayosababisha kuhasirika kwa mwingine.

(ii) Si **lazima** anayetenda tendo hilo la kikatili afaidike moja kwa moja. Mtahiniwa anaweza kujadili tu namna mhusika anavyomdhulumu mwingine **bila kujali**, au kuwazia uchungu anaomsababishia.

7 x 2 = 14

## 3.3 HITIMISHO

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba matokeo ya somo la Kiswahili bado hayajafikia kiwango cha kuridhisha.. Ni watahiniwa wachache mno waliofikia viwango vya juu vya utendaji katika karatasi zote tatu.

Ni matumaini yetu kwamba walimu na wanafunzi watafaidika kwa uchanganuzi uliotolewa. Kadhalika tunawahimiza kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuimarisha matokeo ya somo hili.

## 3.4 MAPENDEKEZO

3.4.1 Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu wake huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:

3.4.2 Dhamira na maudhui

3.4.3 Fani , kama vile:

- Mandhari
- Ploti
- Usimulizi
- Wahusika
- Muundo
- Mtindo, kama vile tamathali za usemi, urudiaji, n.k

3.4.4 Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

3.4.5 Wanafunzi wawekewe msingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza.

3.4.6 Walimu wawafundishe wanafunzi wao istilahi muhimu zinazohusiana na ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya ushairi.